

# HALMASHAURI YA WILAYA YA IKUNGI

(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)

**Mkoa wa Singida:**

**Simu No.** 0262964037/6

**Baruapepe:** ded.ikungidc@singida.go.tz

**Tovuti:** www.ikungidc.go.tz

Baruapepe: ded.ikungidc@singida.go.tz



S.L.P. 42,  
**SINGIDA.**

**Kumb. Na.** IDC/B.1/8/"A"/02

**Tarehe:** 09 Juni, 2020

## TANGAZO LA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi anapenda kuwatangazia waombaji wenye sifa nafasi za kazi za **Mtendaji wa Kijiji Daraja la III.**

### 1. MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III. NAFASI MBILI (02).

Sifa za kuingilia moja kwa moja:

1. Mwajiriwa awe na elimu ya kidato cha nne (IV) au sita (VI) aliyehitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti katika moja ya fani zifuatazo:

- Utawala, Sheria, Usimamizi wa Fedha na Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya jamii kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

#### i. **Kazi/Majukumu ya kufanya:**

- a. Afisa Masuhuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji
- b. Kusimamia ulinzi na usalama wa raia na mali zao, Kuwa Mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala Bora katika ngazi ya Kijiji
- c. Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiji.
- d. Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji
- e. Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu
- f. Kuandaa Taarifa za Utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali
- g. Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya Kitaalam katika Kijiji.
- h. Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za Kijiji.
- i. Mwenyekiti wa Kikao cha Wataalamu waliopo katika Kijiji
- j. Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya Wananchi
- k. Kusimamia utungaji wa sheria ndogo za kijiji.
- l. Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata.

#### **MSHAHARA:**

Ngazi ya Mshahara wa Serikali TGS. **B.1**

#### **MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KWA WAOMBAJI:-**

- i. Waombaji wote wawe raia wa Tanzania ambao hawazidi umri zaidi ya miaka 45 na hawapungui umri wa miaka 18,

- ii. Waombaji wote lazima waambatanishe wasifu binafsi (CV) zenye mawasiliano ya uhakika, anuani, barua pepe na namba za simu.
- iii. Waombaji wote waombe kwa kufuata masharti ya **TANGAZO LA KAZI**,
  
- iv. Waombaji lazima waambatanishe nakala za vyeti vifuatavyo:-
  - a) Astashahada/Cheti cha Utaalamu kulingana na sifa za nafasi husika
  - b) Cheti cha mtihani wa kidao cha nne au sita,
  - c) Cheti cha kuzaliwa.
- v. Hati ya matokeo ya kidato cha nne (Result slip) haitafanyiwa kazi.
- vi. "Transcript" ambayo haikuambatanishwa na cheti haitafanyiwa kazi.
- vii. Kuwasilisha vyeti vya kughushi na maelezo mengine itasababisha kuchukuliwa hatua za kisheria.
- viii. Watumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba nafasi hizi.
- ix. Waombaji ambao walistaafu kazi kwa sababu yoyote ile hawaruhusiwi kuomba nafasi hizi.
- x. Waombaji waonyeshe wadhamini wawili na mawasiliano yao, anuani na namba za simu.
- xi. Waombaji wenye vyeti vya kidato cha nne na cheti cha Taaluma ambavyo vimepatikana nje ya nchi wahakikishe vimehakikiwa na Baraza la Mitihani la Taifa (**NECTA**) na Baraza la Elimu ya ufundi la Taifa (**NACTE**).
- xii. Barua ya maombi iandikwe kwa Kiswahili au kiingereza.
- xiii. Watakaochaguliwa kufanya usaili watajulishwa tarehe ya usaili kupitia tovuti ya Halmashauri – **www.ikungidc.go.tz**
- xiv. Kwa waombaji wenye vyeti vya ngazi ya **NTA level 4 "Basic Technician Certificate" (NTA Level 4)** maombi yao hayatafanyiwa kazi. Kwasasa cheti kinachopokelewa ni **"Technician Certificate" (NTA level 5) na kuendelea**

Mwisho wa kutuma maombi ni **tarehe 23 Juni, 2020 saa tisa na nusu (9:30) Alasiri**. Tangazo hili pia linapatikana kwenye tovuti ya Halmashauri na Sekretarieti ya Ajira.

**Maombi yote yatumwe kwa :-**

**Mkurugenzi Mtendaji,  
Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi,  
S.L.P. 42,  
SINGIDA.**

**(Justice L. Kijazi)**  
MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA  
**IKUNGI**

**Nakala:** Katibu Tawala Mkoa  
Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,  
S.L.P 5,  
**SINGIDA.**

Halmashauri zote,  
Mkoa wa Singida,

Mbao za matangazo Wilaya na Kata.

